

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA NANE**

**27 MEI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE – TAREHE 27 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **316. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mpango wa Serikali kuwawezesha Akina Baba kiuchumi baada ya mpango wa Halmashauri wa kuwawezesha Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu kuwa na mafanikio makubwa.

#### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **317. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali itawasaidiaje Wafanyabiashara wa Dagua wanaofuata Masoko nchi jirani ambao hutozwa ushuru Zanzibar na Tunduma kwa upande wa Tanzania Bara.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**318. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM  
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi linao uwezo wa kukomesha tatizo sugu la ubakaji na ulawiti kwa Watoto wadogo nchini:-

Je, ni kwa nini Serikali isiunde Kikosi Maalum cha kuwashughulikia watu wanaojihusisha na vitendo vya ubakaji na ulawiti.

**WIZARA YA MADINI:**

**319. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE  
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, nini mpango wa Serikali baada ya kukamilika kwa Mradi wa Utafiti wa Madini ya Graphite Kata ya Chiwata.

**WIZARA YA MAJI:**

**320. MHESHIMIWA SIMON SONGE  
LUSENGEKILE (BUSEGA):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-



Je, ni lini Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kutoka Busega mpaka Itilima kupitia Bariadi utaanza kutekelezwa.

**V. HOJA ZA SERIKALI:  
WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA  
27 MEI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**